



KWA AJILI YA VIJANA WETU

Onyesha Usadikisho!

Maagizo: Fanya zoezi hili katika mazingira matulivu. Unaposoma maandiko, jiwazie ukiwa katika matukio yanayozungumziwa. Wazia kikao. Sikia sauti. Hisi kama wahusika wakuu wanavyohisi. Wazia kwamba masimulizi haya ni halisi kabisa.

Wahusika wakuu: Yeremia, Ebed-meleki, Mfalme Sedekia

Muhtasari: Yeremia anapingwa vikali sana anapotangaza ujumbe wa Mungu kwamba watu wa Yuda wanapaswa kujisalimisha kwa Wakaldayo.

① CHUNGUZA TUKIO HILI.—SOMA YEREMIA 38:1-5.

Unafikiri Yeremia alihisi namna gani alipokuwa akizungumza na watu wa Yuda? _____

Unafikiri sauti ya Yeremia ilionyesha hisia gani alipotangaza onyo la Yehova? _____

CHIMBA ZAIDI.

Yeremia alikuwa na usadikisho gani ambao ulimwezesha kutoa tangazo hilo kwa ujasiri?

② CHUNGUZA TUKIO HILO.—SOMA YEREMIA 38:6-13.

Unawazia tangi hilo la maji lilikuwa na umbo, upana, kina, na harufu gani? _____

Huenda Yeremia alikuwa na mawazo gani alipoanza “kuzama katika yale matope”?
(Soma tena mstari wa 6.) _____

CHIMBA ZAIDI.

Ukitumia vifaa vya kufanyia utafiti unavyoweza kupata, chunguza jambo ambalo huku-
jua kuhusu matangi ya maji yaliyotumiwa nyakati za Biblia. _____

Ebed-meleki alisadiki nini alipoomba Yeremia aoko-
lewe? (Soma tena mistari ya 7-9.) _____

Kwa nini Sedekia alishawishiwa kwa urahisi sana,
kwanza na wakuu na baadaye na Ebed-meleki?
(Soma tena mistari wa 5 na 10.) Hilo linaonyesha
nini kuhusu utu wake? jinsi alivyokosa usadikisho?

Ni watu gani katika simulizi hili ambao walionye-
sha usadikisho wenye nguvu, na ni nani ambaye
hakuonyesha? Kwa nini unajibu hivyo? _____

**3 TUMIA MAMBO ULIYOJIFUNZA. ANDIKA
MAMBO ULIYOJIFUNZA KUHUSU . . .**

Ujasiri. _____

Usadikisho. _____

Jinsi Yehova anavyowalinda wale wanaomtii bila
kuogopa. _____

Kuwa na usadikisho kunaweza kukusaidia jinsi gani
kufanya yaliyo sawa unapokabili mkazo? _____

**4 NI MAMBO GANI KATIKA SIMULIZI HILI
AMBAYO YAMEKUGUSA MOYO SANA, NA
KWA NINI?**

